UHAKIKI WA NAKALA YA "DHANA ZA MOFU, MOFIMU NA ALOMOFU

R. Mgullu

MWANDISHI: Ignace B. Marealle

MCHAPISHAJI: TUKI(MULIKA Na. 13(1978))

MHAKIKI: Richard Mgullu

Madhumuni ya makala haya ni kuihakiki makala ya "Dhana za Mofu, Mofimu, na Alomofu" yaliyoandikwa na Ignace B. Marealle na kuchapishwa katika Mulika toleo la 13 la Mwaka 1978. Ni dhahiri kwamba dhana za Mofu, Mofimu na Alomofu ni muhimu katika uchambuzi wa kiisimu na hususani katika eneo la Mofolojia. Kutokana na umuhimu huo tunalo jukumu kubwa la kuzieleza dhana hizi kikamilifu.

DHANA YA MOFU

Katika makala yake, Marealle(1978), ameanza kuifafanua dhana ya Mofu kwa kutoa fasili ya dhana ya Mofu kuwa ni "Vipande vya maneno ambavyo husetiri Mofimu." Ametumia mfano wa neno anaimba kuonyesha kuwa neno hilo limejengwa na Mofu a - na - imb - a.

Anaendelea kueleza kuwa zipo Mofu za aina nyingine ambazo anaziita Mofu dhahania. Anatolea mfano wa neno a-f-a kuwa limejengwa na Mofu dhahania. Kitu ambacho si dhahiri hapa ni kwamba je katika neno afa Mofu dhahania ni zipi? Je! ni a-au-f-au-a? Tukichunguza maana za Mofu hizi tunagundua kuwa hazitofautiani hata kidogo na maana zilizotolewa katika neno anaimba kwani katika neno afa Mofu a- inawakilisha nafsi ya tatu, Idadi ya umoja ya nafsi hiyo, na ni kiambisho cha ngeli ya nomino hiyo.

Mofu - f - ni mzizi wa kitenzi.

Mofu a - ni kiambisho tamati cha kauli

Tofauti iliyopo baina ya neno afa na anaimba ni moja tu yaani kutokuwepo kwa mofu ya wakati (na) katika neno afa

| | | | |
|---|---|---|---|
| a - | na- | imba- | -a |
| a - | - | f- | a |

Kwa msingi huo hakuna sababu yoyote iliyoelezwa ya kuufanya Mofu katika, afa ziwe dhahania na tofauti na mofu katika neno anaimba.

Marealle(Uk 12) anaendelea tena kusema kuwa "kuna mofu nyingine ambazo hutokea katika maneno marefu. Mofu hizi tunaweza kuziita Mofu tata." Halafu ametoa mfano wa neno a-me-ni-chez-e-a. Kwa kweli si sahihi kuziita mofu zilizo katika maneno marefu kuwa ni tata. Kilichotokea hapa ni kwamba neno amenichezea limeundwa na Mofu nyingi na kwa sababu hiyo tunaweza kusema kuwa muundo wa neno hilo ni Changamano(Complex) na siyo kwamba mofu zinazolijenga neno hilo ni tata kwani a katika anaimba au afa au amenichezea ina uamlifu, thamani, na muundo ule ule.

Marealle(uk.12) anaendelea kueleza kuwa "Mofu ambayo ni kiini hapa ni chez ambayo ni shina la neno." Tatizo lililopo hapa ni kule kukiita kiini chez kuwa ni shina, kwani hivi sasa ziko istilahi mbili ambazo hutumiwa kuelezea viini vya maneno, yaani Mzizi na shina. Kwa wakati huu wanaisimu wengi hutumia istilahi ya mzizi kuelezea umbo la msingi(Base form) la neno ambalo halina kiambisho chochote na wanatumia Istilahi shina kuelezea kiini ambacho kimenyambuliwa(kiini zalika). Kwa hiyo chez ni mzizi na siyo shina.

Aidha, Marealle(uk. 12) anaendelea kueleza kuwa katika neno a-me-ni-chez-e-a "Mofu e inaonyesha sababu za kitendo kilichofanyika." Hapa ndipo mahali pekee palipo na utata kwa maana ya kwamba Mofu e ni ya kutendea na kutendea huko kunaweza kuwa na maana zaidi ya moja kama vile:

(1) Kucheza kwa niaba yangu.
(2) Kunifanyia mchezo (mimi).
(3) Kuonyesha sababu za kunichezea.

Kwa msingi huo mofu tata katika neno amenichezea ni e peke yake.

Katika para ya nne(uk. 13) Marealle anadai kuwa "Hata hivyo kuna maneno ambayo hayana Mofu kwa mfano baba." Hoja-

hii si sahihi kwani tumekwisha kusema kuwa mofu ni maumbo yanayosetiri maana na kwa kuwa kila neno huwa na maana, basi, kila neno lazima huwa na mofu. Miundo ya maneno hutofautiana. Yapo maneno ambayo miundo yake ni sahili kwa maana ya kwamba maneno hayo huundwa na mofu moja tu, kwa mfano, baba, mama, na, ni, ili n.k. Aidha, yapo maneno yenye miundo Changamano ambayo huundwa na zaidi ya Mofu moja. Tutakuwa tunakosea kusema kuwa maneno "mama, baba, na, ili" na mengine hayana mofu kwani maneno hayo yanaundwa na mofu moja moja ambazo husetiri maana zilizopo katika maneno hayo nayo huweza kuongezewa Mofu zingine kwa mfano,, mamake, babangu, naye n.k.

DHANA YA MOFIMU

Marealle(uk. 13), anaeleza vizuri kuwa "Mofimu ni kipashio kidogo kabisa cha kisarufi kilicho na maana." Akaendelea kutoa mifano kuwa:

(a) a - na - tembe - a Mofimu 4
(b) wa - na - pig - a - na - Mofimu 5
(c) a - na - kimbi - a - Mofimu 4

Kwa kuitumia mifano hii mitatu, ni vigumu sana kutofautisha mofu na mofimu. Mofimu ni maana iliyopo katika Mofu fulani na kwa hali hiyo mofimu ni dhana dhahania na si sehemu ya neno. Katika mfano (a) hapo juu.

(a) a - na - tembe - a - kuna Mofimu 6 na siyo 4
yaani -

(1) a - inawakilisha nafsi ya tatu.
(2) a - inawakilisha umoja.
(3) a - inawakilisha ngeli ya yu - a - wa.
(4) na - wakati uliopo/kuendelea.
(5) tembe - mzizi wa kitenzi.
(6) a - kiambishi tamati cha kauli yakinishi.

Katika mfano wa (b) hapo juu kuna mofimu 7 na siyo 5.

(b) wa - na - pig - an - a

(1) Wa - inawakilisha nafsi ya tatu.
(2) Wa - ina wakilisha idadi ya wingi.
(3) Wa - inawakilisha ngeli ya yu - a - wa(MU-WA).
(4) na - wakati uliopo/kuendelea.
(5) - pig - Mzizi wa kitenzi.
(6) - an - inawakilisha kutendana.
(7) a - kiambisho tamati cha kauli yakinishi.

Hapa tunagundua kuwa hata ule mgawanyo wa mofu za neno Wa-na-pig-a-na ni wa makosa kwani mgawanyo sahihi ni Wa-na-pig-an-a ambapo an ni mofu moja.

Katika mfano wa (c) hapo juu, katika neno a-na-kimbi-a kuna mofimu sita na siyo nne, yaani:-

(1) a - inawakilisha nafsi ya tatu.
(2) a - inawakilisha idadi ya umoja.
(3) a - inawakilisha ngeli ya yu-a-wa(MU-WA).
(4) na - wakati uliopo/kuendelea.
(5) kimbi - mzizi wa kitenzi.
(6) a - kiambisho tamati kauli yakinishi.

Kinachojidhihirisha kutokana na mifano hii mitatu ni kuwa kila mofu huwa na maana moja au zaidi. Katika Lugha ya Kiswahili mofu ambazo huwekwa mwanzoni mwa vifungutenzi kwa mfano: a, - wa, n.k. aghalabu huwa na maana zaidi ya moja.

Hapa tunaona ya kuwa katika mifano mitatu(a - c) hapo juu, zile alizoziita mofimu kwa kweli si mofimu bali ni mofu.

Kwa hiyo katika:-

(a) a - na - tembe - a kuna mofu 4 na mofimu 6.
(b) wa - na - pig - ana kuna mofu 5 na mofimu 7.
(c) a - na - kimbi - a - kuna mofu 4 na mofimu 6.

Katika ukurasa wa 14 Marealle akielezea uhusiano uliopo baina ya viambisho na mofu anaeleza kuwa "katika neno a - na -sem-a a ambayo ni kiambisho awali inawakilisha Umoja na nafsi ya tatu, pili inawakilisha idadi, tatu inawakilisha Umoja na nne huwa ni mofu. Hapa tunaona kuwa mofimu ya idadi imetajwa mara tatu na haya ni makosa. Maelezo sahihi yangekuwa kwamba:-

(1) a - inawakilisha nafsi ya tatu.
(2) a - inawakilisha idadi ya umoja.
(3) a - inawakilisha ngeli ya YU-A-WA.

Hatuna haja ya kusema kuwa a ni mofu kwani kuwa mofu siyo maana.

Kaida ambayo imejidhihirisha katika lugha ya Kiswahili ni kuwa mara nyingi idadi ya mofu itakuwa ndogo kuliko idadi ya mofimu kutokana na baadhi ya mofu katika Kiswahili kuwakilisha mofimu zaidi ya moja.

ALO ni kiambisho awali ambacho hutumiwa na wanaisimu kuelezea mabadiliko ambayo hutokea katika umbo la kipashio hicho. Mabadiliko ya aina hii ambayo yamekuwa yakijadiliwa sana na wanaisimu ni pamoja na:-

(1) Alografu(allograph) - yaani maumbo mbalimbali ya herufi(graph) moja. Kwa mfano, herufi kubwa na herufi ndogo /A/ na /a/ au /B/ na /b/.

(2) Alofoni(allophone) - yaani maumbo mbalimbali ya fonimu moja.

(3) Alomofu(allomorph) - yaani maumbo mbalimbali ya mofimu moja.

Maelezo haya yanafanana sana na yale anayoyatoa Marealle (uk. 14) kuwa "Wakati inapotokea mofimu moja kuwa na maumbo mbalimbali ndipo tunapopata dhana ya alomofu." Katika kuonyesha jinsi alomofu zinavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili, Marealle(Uk. 11) ametumia mfano wa kiambisho MU - cha umoja katika nomino za ngeli ya YU-A-WA na kuonyesha kuwa mofu MU ya umoja huweza kujidhihirisha kwa alomofu hizi:-

(i) MU - kama katika - MU - undo (Muundo)
(ii) M - kama katika - M-tu (Mtu)
(iii) MW - kama katika - Mw-erevu (Mwerevu)

Hapa tungeweza pia kutumia mfano wa mofu - ISH - ambayo huwakilisha hali ya kutendesha. Imebainika kuwa katika lugha ya Kiswahili mofu ISH hubadilikabadilika kutegemea umbo la kitenzi; kwa mfano:

(1) Mizizi ya vitenzi yenye irabu, a, i, na u hutumia mofu - ISH - k.m.:

(a) Pata → patisha (ish)
(b) Shika → shikisha (ish)

(2) Mizizi ya vitenzi yenye irabu ya e au c hutumia mofu - esh k.m.:

(a) kopa → kopesha (esh)
(b) cheza → chezesha (esh)

(3) Mizizi ya vitenzi yenye silabi moja tu na ambayo huishia na mfululizo wa irabu mbili hutumia mofu - z k.m.:

(a) toa - toza (-z-)
(b) lia - liza (-z-)
(c) paa - paza (-z-)
(d) jaa - jaza (-z-)

(4) Mizizi mingine ya vitenzi yenye silabi moja na kuishia na irabu mbili mfululizo hutumia mofu - lish - k.m.:

(1) Zaa - zalisha (lish)
(2) Kaa - kalisha (lish)
(3) Vaa - valisha (lish).

Kwa mifano hiyo tunagundua kuwa mofimu ya kutendesha huweza kudhihirishwa kwa kutumia alomofu nne yaani:-

| | | |
|---|---|---|
| ( (1) | - ISH - ) | |
| ( (2) | - ESH - ) | alomofu za |
| ( (3) | - Z - ) | mofimu ya |
| ( (4) | -LISH - ) | kutendesha. |

HITIMISHO

Dhana za mofu, Mofimu, na Alomofu zinahusiana, na kukaribiana sana. Mofu ni maumbo ambayo huonekana dhahiri katika maneno. Ni viambajengo vya maneno. Mofu ni maumbo ambayo hubeba maana(Mofimu) fulani. Mofimu ni maana ambazo husetiriwa kwenye Mofu. Mofimu ni dhana dhahania na hazipo kwenye neno. Mofimu si sehemu ya neno. Katika mofu moja panaweza kuwepo mofimu(maana) zaidi ya moja. Alomofu ni maumbo mbalimbali mofimu moja. Mofimu ya kutendesha katika Kiswahili, kwa mfano, huweza kuwakilishwa na alomofu (-ISH-), (-esh), (-z-), au (-lish-).

MAREJEO

(1) Brown E.K. & Miller, J.E. Syntax. A linguistic Introduction to sentence structure

(2) Gleason(1969) An Introduction to Descriptive Linguistics. Holt, Rinehart & Winston

(3) Lyens J.(Ed) (1970) New Horizons in linguistics. Pelican.

(4) Mathews, P.H.(1974) Morphology Cambridge University Press.

(5) Nida, E.(1971) Morphology. University of Michigan.